

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
31 Januari 2009**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Beda John Mkusu
Filbert Mbecha
Idrisa Kessi Zongo
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Jumanne Ayuba
Kassim Bakari
Mohammed Samwely
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Selion Elieskia
Shamte J Kigoma
Shukuru Hassan
Sosthenes C Amlima

Ruzuku ya Foundation for Civil Society

Juma Chibaya alipata barua ya serikali ya mtaa. Serekali ya mtaa wametaka wapelekewe nakala ya katiba na majina ya viongozi, na Juma Chibaya aliwaletea.

Paulo alitembelea Bwana Gaja na Diwani Lupilya kuwaomba kuwa wadhimini huru. Diwani Lupilya alijibu kwa barua kwamba amekubali na alitupa ushauri kuhusu vipi kuendesha mradi. Bwana Gaja amejibu kwamba ataleta yeye mwenyewe jibu kwenye ofisi yetu.

Hatujapata taarifa yeyote kutoka kwa Hamadi Bwaja kwa sababu hakuja kwenye mkutano.

Mkutano na SUMATRA

SUMATRA walitangaza mkutano kuhusu nauli za mabasi. Juma, Filbert na Sosthenes walihudhuria.

Ushirika wa kibarua wa baisikeli

Idrisi alikwenda ofisi ya ushirika mkoa kupata maelezo juu ya kuanzisha ushirika. Jibu – ameambiwa kwamba iandikwe barua ya kuomba maelezo na siyo maelezo ya mdomo.

Shukuru alitembelea ofisa ya ushirika Kinodoni – Bwana Bukuku alikini ameambiwa na arudi tena baada ya wiki moja kwani amefiwa na mwanee amekwenda msiba.

Video ya usalama wa baisikeli

Sosthenes amepata mtu wa kutoa DVD. Anataka ajue idadi ya DVD tunazotaka kuzitoa maana zikiwa zaidi ya kumi kuna kuwa na punguzo la bei.

Mambo ya hela na guta

Dereva wa guta Ramadhan Nyengo amelipa Tsh 7,000 ya wiki hii.

Guta linatakiwa linunuliwe vifaa kama vile a) balling 2, kila belling Tsh 4,000 x 2 = Tsh 8,000, b) ngao 2 kila ngao Tsh 3,000 x 2 = Tsh 6,000. Jumla Tsh 14,000. UWABA imekopeshwa pesa za kununulia vifaa vya guta Tsh 14,000 kutoka kwa mwanachama Shukuru Hassan.